

# Usambazaji wa Kondomu

Idara ya Afya ya Wilaya ya Allegheny inaweza kutoa bidhaa za ngono zilizo salama zaidi bila malipo (aina tofauti za kondomu za kiume, vifaa vya kukinga mdomo wakati wa ngono, na mafuta ya kulainisha) kwa watu binafsi au mashirika ambayo huwasilisha ombi. Mpango wa usambazaji kondomu husambaza kondomu na vitabu kwa jamii na mashirika katika wilaya nzima ya Allegheny. Iwapo ungependa kujifunza zaidi kuhusu mpango huu au kupokea bidhaa za ngono zilizo salama zaidi za bila malipo kupitia Mpango wetu wa Usambazi Kondomu, tafadhali wasiliana na CDP@AlleghenyCounty.us



## Kliniki ya Afya ya Umma ya Idara ya Afya ya Wilaya ya Allegheny

1908 Barabara ya Wylie (Mkoa wa Hill)  
Pittsburgh, PA 15219

412-578-8081

[www.achd.net](http://www.achd.net)

### Saa za Kliniki

Jumatatu, Jumanne, Alhamisi, Ijumaa 8:30  
asubuhi. - 3:30 alasisiri

Jumatano 12:30  
adhuhuri. - 7:30 usiku

Kujisajili kutaanza dakika 30 mapema zaidi

Idara ya Afya ya Wilaya  
ya Allegheny

# Kliniki ya Afya

Uchunguzi na  
Matibabu ya  
Virusi vya  
Ukimwi BILA  
MALIPO

# Know your status.

Get tested.

## Uchunguzi wa Virusi vya Ukimwi Bila malipo na wa Siri

Idara ya Afya ya Wilaya ya Allegheny hutoa Uchunguzi wa virusi vya ukimwi bila malipo na wa siri. Sisi ni kliniki bila malipo na ya siri unayoweza kuingia wakati wowote. Hakuna miadi au bima inayohitajika. Kila aliye na umri wa mika 13 na zaidi anaweza kuhudumiwa katika kliniki yetu, bila kujali hali yake ya uhamiaji. Idhini ya mzazi haihitajiki.

Kliniki yetu hufanya uchunguzi wa virusi vya ukimwi, klamidia, kisonono na kaswende. Iwapo mgonjwa atatambulika kuwa na klamidia, kisono au kaswende atapokea matibabu papo hapo. Iwapo una dalili uchunguzi zaidi unaweza kufanyika. Wagonjwa waliotambuliwa kuwa na virusi vya ukimwi watapokea rufaa ya utunzaji wa afya. Sisi pia hutoa rufaa ya profilaksisi ya Kuzuia uambukizaji (PrEP).

Huwaomba wagonjwa kuja na picha ya kitambulisho. (yaani leseni ya uendeshaji gari, pasipoti, Kitambulisho cha chuo) wakati wa kuhudumiwa. Iwapo huna picha ya kitambulisho utahudumiwa tu, lakini picha ya kitambulisho inahitajika ili kupata matokeo.

## Kliniki ya Afya ya Umma Hufanya Uchunguzi Ufuatao:

Kliniki ya Magonjwa ya Zinaa hufanya uchunguzi ufuatao wa maambukizi ya Zinaa na bakteria

- Uchunguzi wa Virusi vya Ukimwi (damu)
- Kaswende (damu)
- Klamidia
- Kisonono
- Trikonomiasisi (uchunguzi wa ukeni tu)
- Chachu (uchunguzi wa ukeni tu)
- Vajinosisi ya bakteria
- Inflammesheni ya Urethra isiyoyana Gonokokasi (NGU) (swabu ya uume tu)
- Hepatitisi A, B, C (uchunguzi wa tita wa kupima kinga):  
(Ada: Dola 25 wakazi wa Wilaya ya Allegheny na Dola 30 wasio wakazi wa Wilaya ya Allegheny)
- Upele (matibabu tu)
- Chawa ya kinena (matibabu tu)
- Malengelenge ya ngozi (hatufanyi uchunguzi wa damu, lakini tutafanya uchunguzi wa vimelea iwapo majeraha yapo).



## Kliniki ya Afya ya Umma HAIFANYI Uchunguzi wa Yafuatayo:

- Maambukizi ya Njia ya Mkojo (UTI)
- Virusi vya Papiloma vya Binadamu (HPV)
- Mimba
- Uchunguzi wa Kimwili
- Uchunguzi wa haraka wa Virusi vya Ukimwi

## Huduma za Ushirika

Wafanyakazi wa Idara ya Afya ya Wilaya ya Allegheny wanaweza kuwajulisha wapenzi wa kingono wa wagonjwa walio na utambuzi chanya wa Magonjwa ya Zinaa waje kwa uchunguzi na matibabu ya siri na yasiyo ya malipo ya Virusi vya Ukimwi/Magonjwa ya Zinaa.

Hii ni huduma ya kujitolea kwa kila aliyetambuliwa kuwa na Ugonjwa wa Zinaa. Wafanyakazi hawafichui utambulisho au habari yoyote ya utambuzi kuhusu mgonjwa wanapowajulisha wapenzi.

Arifa ya mpenzi hufanya kazi ili kuzuia kuenea kwa Virusi vya Ukimwi/Magonjwa ya Zinaa katika Wilaya ya.

### Rasilimali Zaidi

Rasilimali za Magonjwa ya Zinaa za Idara ya Afya ya Wilaya ya:

[www.achd.net/std](http://www.achd.net/std)

Kituo cha Udhhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa Rasilimali za Magonjwa ya Zinaa:

[www.cdc.gov/std](http://www.cdc.gov/std)

Jifunze kuzungumza na mpenzi wako kuhusu ngono na Magonjwa ya zinaa:

[www.gytnow.org/talking-to-your-partner](http://www.gytnow.org/talking-to-your-partner)

Habari kuhusu PrEP:

[www.preppgh.org](http://www.preppgh.org)